



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na: MTC/I.20/2/155

01/06/2023

## TANGAZO LA NAFASI LA KAZI ZA VIBARUA WA KUKUSANYA MAPATO HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO.

Mkurugenzi wa Mji, Halmashauri ya Makambako anapenda kuwatangazia watazania wote wenye sifa tajwa hapo chini kuomba nafasi za kazi za vibarua wa kukusanya mapato ya Halmashauri ya Mji makambako katika nafasi zifuatazo:

### MWOMBAJI ANATAKIWA KUOMBA NAFASI MOJA TU KATI YA NAFASI ZIFUATAZO

1. Nafasi ya kibarua wa kukusanya mapato ya Halmashauri nafasi - 36
2. Nafasi ya kibarua wa kukusanya mapato ya TARURA nafasi - 12

### A) SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe Raia wa Tanzania
- Awe na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18
- Awe anajua kusoma na kuandika
- Awe muadilifu
- Awe mwaminifu ambaye hajawahi kushtakiwa kwa kosa la upotevu wa mapato, hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai.
- Awe na uzoefu wa kazi ya ukusanyaji mapato

- Awe mkazi wa Halmashauri ya Mji Makambako
- Awe tayari kufanya kazi katika eneo lolote atakalopangiwa la Halmashauri ya Mji Makambako.
- Awe tayari kufanya kazi kwa masharti ya kibarua kwa aina ya nafasi ya kazi ya kibarua wa kukusanya mapato atakayochagua kuomba kati ya nafasi Na. "1" au "2" hapo juu

## **B) MAELEKEZO YA JUMLA**

1. Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambatanisho vifuatavyo

- Cheti cha kuzaliwa/Kitambulisho cha NIDA/Uraia /Mpiga kura
- Barua za maombi zipitishwe kwa Watendaji wa Mtaa/Vijiji mwombaji anapoishi
- Picha ndogo (2) za (passport size) za hivi karibuni
- Wasifu binafsi (CV)


2. Awe na wadhamini wawili wenye makazi ya kudumu Halmashauri ya Mji Makambako.

Maombi ambayo hayakidhi vigezo hapo juu hayatashughulikiwa

**C) Mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe 08/07/2023**

Barua zote za maombi zitumwe kwenye anuani ifuatayo

**Mkurugenzi wa Mji,  
Halmashauri ya Mji Makambako,  
S. L.P 405  
MAKAMBAKO.**



Eliud H. Mwakibombaki

MKURUGENZI  
HALMASHAURI YA MJI  
MAKAMBAKO

Kaimu: **MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI**